**MWONGOZO WA KIDATO CHA NNE**

**KISWAHILI FASIHI 102/3**

**SEHEMU YA A: USHAIRI**

a) i) Mwandishi anadhamiria kutuonyesha jinsi watoto wanadhulumiwana
ii) kunyimwa haki na wazazi/watu waume
zozote 2 x 1 = 2

b) Tamathali nne za usemi
   i. Tashibihi – mwafa ja nzi, kama mbwa
   ii. Methali – ngoja , mesikia, inaumiza matumbo
   iii. Msemo – kupuliza mbiu – kutangaza
   iv. Jazanda – jehanamu tumeona
   Za kwanza 4 x 1 = 4

c) Nafsineni ni mtoto
1 x 1 = 1

d) Bahari
   i. Tarbia – mishoro 4 katika kila ubeti
   ii. Pindu – utao wa mstari wa mwisho kuanza ubeti
   iii. Ukaraguni - hakuna urariwa vina
   iv. Manthawi – kila mshororo una vipandi viwili
   v. Sabilia – halina kibwagizo lina kimalizio
   Za kwanza 4 x 1 = 4

e) Ubeti wa 4 kwa lugha nathari
   - Wanauliza ni lini wataacha kunywa pombe haramu
   - Wazazi wote baba na mama wanakunywa bila kuwajali
   - Wanakufa kama nzi nuia kuwaachia matatizo
   - Kwa nini hawaoni/hawatambui ukweli huu
   4 x 1 = 4

f) Maudhui
   - Watoto ni Baraka katika jamii
   - Watoto wanaumia kwa matendo maovu
   - Madhara ya wazazi kunywa pombe
   - Watoto kupigwa vibaya na wazazi wao
   - Anakashifu ubakaji unaotekelezwa kwa watoto wa kike
   ya kwanza 3 x 1 = 3

g) Uhuru wa kishairi
   - Inkisari – mesikia –nimesikia.
   - Kufinyanga sarufi – jehanamu tumeona- tumeona jehanamu
   - Ritifaa – nyi – nyinyi
   Za kwanza 1 x 2 = 2 Kutaja 1, Mfano 1

**SEHEMU YA B: RIWAYA KIDAGAA KIMEMWOZEA**

2. "Dunia imepasuka ufa mkubwa usiozibika alaa kulihali"

a i) Haya ni maneno ya Ben Bella
ii) akimwambia Masheko
iii) Kupitia kwa barua
iv) Ben Bella anasema kauli hii kutokana na uovu wa babake ambao ameufichua kwa Mashaka. Mashaka anahuzunishwa sana na kitendo hiki.

4 x 1 = 4

b) Eleza mbinu mbili za lugha zilizotumika.

i. Chuku – Dunia inasemwa kupasuka ufa mkubwa. Ben Bella anatumia maneno haya kuadhirisha uzito wa maovu ambayo yanatendeka duniani. Maovu yaliyo duniani ni mengi sana kiasi kwamba maadili yamesahaulika kabisa.
ii. Msemo – alaa kulilahi. Kumaanisha kwa vyovyote vile. Maovu yanayotendeka duniani hayawezi kuzuiliwa kwa vyovyote vile. Anasisitiza cha kiwango cha kuporomoka kwa maadili katika dunia.

iii. Jazanda pasuka ufa - uovu anaotokea (za kwanza mbili)2x2=4

c) Thibitisha ukweli kuwa dunia imepasuka ufa mkubwa usiozibika kwa kumulika matukio riwayani. (alama 12)

i. Wananchi wanyang'anywa mashamba yao hadharani. Hakuna wa kuwasaidia.
ii. Wanafunzi wanashiriki mapenzi na walimu wao k.m Mwalimu mkuu anacheza mchezo wa kibe na wanafunzi wake naye Fao anamringa mwanafunzi wake.
iii. Wazazi kupuuza malezi yao wanao – Mtemi anampngaza Amani kitoto Uhuru.
iv. Polisi kutesa raia badala ya kuwapa ulinzi.
v. Maafisa wa mahakama kupokea hongo.
vi. Wahariri kuiba na kuichapisha miswada kwa majina yao.
vii. Wauguzi kupuuza wajibu wao. Hata wanawadhilhakji badala ya kuwahudumia.
viii. Dini kuwa hifadhi ya maovu.
ix. Watoto walemavu kudhalilishwa na wazazi wao k,m Mwalimu Majisifu na mkewe wanawaficha badal yakuwaonyesha mapenzi ya wazazi.
x. Walimu walevi kupewa jukumu la kufundisha wanafunzi.
xi. Viongozi katili kuendelea kushikilia nyadhifa za uongozi.
xii. Ulanguzi wa dawa za kulevya.
xiii. Dj kutohudumiwa anapoumwa na jibwa.
xiv. Viongozi/mtani kuwa na uhusiano na Lowela.

12 x 1 = 12

3. Uchochole umekithiri katika jamii anayotuchorea mwandishi. Thibitisha kauli hii kasha utambue chanzo chake

i. Mavazi yake Amani yanaashiria uhitaji. Saruali yake ni kuukuu iliyo na viraka vikubwa . mavazi ni mojawapo ya mahitaji ya kimsingi ya binadamu.
ii. Maelezo kumhusu Dj yanajenga taswira ya kimaskini. Inaeleza huwa ni kijana mkondefu. Alionekana kukosa mahitaji kama mlo na matibabu.
iii. Umaskini ndio uliosababisha mamake Dj kuishji mtaa wa Madongoromoka na
iv. kupika pombe haramu
v. Amani pamoja na wafanyakzai wengine wanaishi kwenye vibanda uchwara.
vi. Blanketi alilokuwa akitumia lilikuwa na mianya mikubwa na kutoa harufu mbaya.
vii. Watoto wa maskini walishindwa kuendelea na masomo yao kutokjana na ukosefu wa karo.
viii. Kuna maskini wengi Sokomoko waliogawiwa mashamba na Madhubuti / Amani
ix. Watoto wadogo kama Dj kufanya kazi ya uchangaji.
x. Kuna misaada ya kusomesha watoto maksini.
xi. Kina Makweche wanaishi kwenye vibanda.
xii. Mama mjamzito kujifungulia barabarani.
xiii. Watu kutumia dawa za kiasili AK.m Amani alitibiwa na Imani kwa mitishamba naye Dj alitibiwa na mchunga kwa dawa zizo hizo baada ya kutoroka zahanatini.
xiv. Matuko Weye anaishi maisha ya kimaskini. Mwishowe anatafutiwa daktari na Amani. zozote 10 x 1 = 10

Chanzo cha kukithiri kwa umaskini huu

i. Ukosefu wa ardhi kutokana na unyakuzi.
ii. Ukosefu wa elimu-watoto wachungaji hawakuwa na elimu. Aidha, elimu ya kina Imani na Amani ilikatizwa.
iii. Ujira duni.
iv. Ufisadi – Mtemi alikuwa radhi kutoa hongo ili mwanawe apate kazi jeshini.
v. Uyatima – k.m Amani na Imani walikuw mayatima.
vi. Wizi k.v wa miswada - Amani hakufaidika kutokana na mswada alioundaika; aliyefaidka ni Mwalimu majisifu.
vii. Watu kunyamaza badala ya kutetea haki zao.
viii. Ufadhili usiofa.
ix. Utekezaji/matuko/makweche
x. Utepetevu wa viongozi
xi. vifo/wazazi wa Imani
10 x 1 = 10

**SEHEMU YA C: TAMTHLIA KIGOGO**

**4. "Oooh bebi, miaka yaenda mbio sana, nayo sura yako inachujuka……"**

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

i. Ni wimbo wa Kabaka anaouimba Ngurumo.

ii. Anamwimbia Tunu

iii. Wako Mangweni, mahala pa ulevi.

iv. Alikuwa anamdhihaki Tunu na wanaharakati wengine kuwatembelea ili kuwahamasisha kuhusu utawala dhalimu wa Majoka na kuwa ni vyema waupinge.

Hoja zozote 4 x 1 = 4

b) Mhusika anayehusishwa na wimbo huu ana msimano gani wa kimapindjuzi? (alama 8)

i. Ana msimano thabiti. Tunu anasimama kidete bila uoga kupambana na udhalimu wa utawala wa Majoka.

ii. Ni mfano bora wa watu wa jamii; kuwajibika na kuchukua jukumu la kuikomboa jamii inayokandamizwa.

iii. Anafanikiwa kushawishi wananchi wasihudhurie sherehe za uhuru na badala yake wakusanyike katika eneo la soko la Chapakazi ili wadai uhuru wa kweli

iv. Mateso ya kupigwa na kudhulumiwa na utawala havikatizi ari yake katika kuleta mapinduzi.

v. Baadaye kutona na jitihada zake pamoja na wanaharakati wengine, uongo wa Majoka unaondolewa na soko linafunguliwa tena.

vi. Anakataa kuozwa kwa lazima.

vii. Jasiri hamwogopi Majoka .

viii. Mwanaharakati.

Hoja zozote 8 x 1 = alama 8

c) Taja sifa zozote NANE za mhusika huyu (alama 8)

i. Jasiri na mkakamavu.

ii. Mwenye busara.

iii. Mwenye msimamo thabiti.

iv. Ni mzalendo mwenye mapenzi ya dhati kwa nchi yake.

v. Mshawishi.

vi. Mwajibikaji.

vii. Msomi.

viii. Mwenye utu /mkarimju.

ix. King'ang'anizi – aling'ang'ania kudai haki mpaka akaangusha utawala wa Majoka.

x. Mzalendo

xi. Mtetezi

Za kwanza 8 x 1 = Alama 8

5. Tamthilia ya ‘Kigogo’ ni kioo cha uhalisia wa maisha y ajamii nyingi za kiafrika. Thibitisha. (alama 20)

Majibu

Kioo ni kifaa ambacho watu hutumia kutazama sura zao. Watu wakiona sura zao zina kasoro Fulani hulazimika kurekebisha kasoro hiyo kabla hawajatokea mbele za watu. Tamthilia yak Kigogo inatumika kama kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za kiafrika kwa sababu imemulika sura za jamii hizo.

Tamthilia hiyo imeweza kuonyesha kasoro mbalimbali zilizomo katika jamii hizo. Kasoro hizo ni pamoja na:

1. Uongozi mbaya – huu ni uongozi ambo hautilii maanani maslahi ya wananchi wote. Uongozi wa Majoka haujali haki za raia, hauheshimu katiba wala kujali uhuru wa vyombo vya habari.
2. Mauaji ya watu – Katika jimbo la Sagamoyo kuna mauaji ya watu wasio na hatia. Majoka anahusika katika mauaji ya mpinzani wa kiasiasa Jabali. Majoka anapanga njama za kumuua Tunu, kisha Chopi, kuna mauaji ya waandamanaji n.k
3. Usaliti –jimbo la Sagagamoyo limesalitiwa na viongozi walioko madarakani. Badala ya kushughulikia matatizo ya wananchi, wanashughulikia mahitaji yao. Kuna usaliti pia wa ndoa. Mamapima anamsaliti mumewe kwa kjuto uroda ili apate mradi wa kuoka keki ya uhuru. Hii ni kasoro ambayo inajidhihirisha.
4. Ulipaji wa visasi – kiongozi wa Sagamoyo anaongoza kwa visasi. Anamtia Ashua nguvuni ili alipe kisasi kwa Sudi ambaye hataki kumchongea kinyago. Aidha, ana kisasi kwa Sudi kwa kuwa ameoa mrembvo hurulaini ambaye Majoka alimpenda. Kasoro hii inajibainisha katika uhalisia wa jamii nyingi za Kiafrika.
5. Suala la migogoro – tamthilia hii imebainisha kuwapo kwa migogoro anuwai katika jimbo la Sagamoyo. Kuna mgogoro kati ya kundi la Tunu dhidi ua kundi la watawala. Mgogoro huu unachochewa na kitendo cha Tunu kuongoza Wanasagamoyo kudai haki zao. Suala hili linasawirika katika jamii nyingi za Kiafriaka.
6. Ubinafsi na ukiritimba – Hii ni hali ya mtu kujali mambo yake tu bil kufikiria mambo ya mwingine. Utawal wa Majoka ni wa kibinafsi na ukiritimba. Wanafunga soko la Chapakazi kwa manufaa binafsi.
7. Ukoloni mamboleo – Ukoloni mamboleo unajitokeza katika mambo yafuatayo. Kwanza, kutegemea misaada kutoka nchi za kigeni ni kuendeleza ukoloni mamboleo. Utawala wa Majoka unapokea mkopo kutoka mataifa ya kigeni. Mkopo huo unatakiwa kulipwa kwa miaka mia moja.
8. Athari za ulevi na dawa za kulevya – jimbo la Sagamoyo limejaa vijana wenye uraibu wa kulew pombe haramu. Ngurumo na walevi wenzake wanaonekana kuraibu pombe haramu inayouzwa na mamapima mangweni. Aidha, wanafunzi katika shule za Majoka and Majoka Academy wna uraibu wakutumia dawa za kulevya.
9. Matumizi ya vikaragosi – vijana walevi wanazugwa akili kuhusu Majoka. Wanataka kumpigia kura na hawataki mtu mwingine. Kura yangu simpi mtu mwingine kama si Majoka heri nimpe paka wake

10. Ufisadi – Ngurumo anadai kuwa wtu wa kigogo hupitia pale wakakawarushia kitu (wanapewa vijisenti) Vikaragosi wengine kama Kenga anaota ushauri mbaya kwa Majoka ili kujunufaisha. Anafaidi kutokana na kufungwa kwa soko la Chapakazi kwa kutengewa kiwanja. Hoja zingine ni pamoja na
11. Matumizi mambaya ya vyombo vya dola – askari jela kama Chopi ni mpyaro na katili
12. Unyakuzi wa ardhi- Majoka ananyakua uwanja wa soko la Chapakazi ili ajenge hoteli ya kifahari.
13. Kuangamiza wapinzani – Jabali aliuawa kwa hila za Majoka ili asimpinge, aidha chama chake cha Mwenge kikafifia pia.
14. Tenga tawala – Majoka amegawanya watu ili awatawale kwa urahisi. Ngurumo anarejelewa na Chopi kama mtu wetu.
15. Elimu duni – Wanafunzi wanatumia dawa za kulevya na wamekuwa dhaifu – makabeji.
16. Utawala wa kiimla – Majoka anatawala kwa kutumia mabavu.
17. Ulevi – Kule mangweni kuna vijana kama Ngurumo na mtu wa I na wa II ambo wameathirika mno kwa ulevi; hawana akili razini.
18. Matabaka – Kuna vigogo wenye mali nyingi na walala hoi wasio na mali mfano wachonga vinyago hula makombo ya keki ya uhuru.
19. Ukosefu wa uajibikaji – kuna njaa – kutokana na kufungwa kwa soko watoto wa Sudi wanateseka kwa njaa.
20. Viongozi wanafuja mali ya umma – Kenga anamrubuni Sudi kwa fedha nyingi.
21. Hakuna huduma za afya – Mandhari ya soko ni machafu na Sudi anasema kuwa watu wanasumbuliwa na aina nyingi za ndwele.
22. Uharibifu wa mazingira.

Hoja zozote 20 x 1 = 20

**<u>SEHEMU YA D: HADITHI FUPI TUMBO LISILOSIMBA NA HADITHI NYINGINEZO</u>**

**6. "Rasta twambie bwana!"**

a) Weka dondo katika muktadha
   - Maneno ya wanafunzi wa shule ya Busulala.
   - Akimwambia Rasta/ Samueli Matandiko.
   - Walipokuwa shuleni.
   - Samueli alikuwa ametoka katika afisi ya mwalimu mkuu kuchukua matoke yake ya mtihani. Marafiki waliomjua wanamtaka awaelezee alama zake.
     (Alama 4)
     4x1=4

b) Taja mbinu iliyotumiwa na mwanafunzi katika dondoo hili
   i)Utohozi ii)nidaa (alama 1x1)

c) Ni kwa vipi mzungumziwa anamchukulia mwalimu mkuu kama hambe?

- Mwalimu mkuu wa shule ya Busukalala hakuwahi kumwamini Samueli hata siku moja kama anaweza kufaulu mtihani

- Mwalimu mkuu hakuamini Samueli aliposema kuwa amelipa ada mpaka alipohakikisha kwa kuangalia nyaraka na kumbukumbu zake.
- Anamwonyesha Samueli dharau kwa mumrisha karatasi kama mbwa; anarejelea kile alichokuwa akifanya na kumpuuza.
- Mwalimu mkuu hakumpa ushauri wowote Samueli ambo unmgemsaidia kupokea matokeo yake ambayo hayakuwa mazuri hata kidogo.
- Mwalimu mkuu alimjibu Samueli kwa karaha, alipomwita kuwa ni fidhuli.  Anamjibiza kwa kuuliza iwapo wanafunzi wengine wanalipa mawe au majani.

zozote 5x1

d) Je, mtihani wa maisha ni amwani faafu yua hadithi hii.
  - Mtihani wa Maisha ni anwani ambaayo imesawiri maudhui ya hadithi hii kwa kiwango kikubwa.
  - Samueli anafanya mtihani wake wa shuyle ya upili na kuend kuyachukua matokeo. Kabla ya kufikia zamu zake Samueli anajichjunguz na kujipima uwapo ameufanya vizuri.  Mawazo kuhusu mtihani huo yanamtawala.
  - Alianza kuwachunguza wanafunzi waliokuja kuchukua matokeo ya mtihani wanaopotoka mlangoni ili kujaribu  kuona iwapo wamefaulu au la.
  - Samueli anajaribu kujiaminisha kuwa yeye atakuwa amefaulu mtihani wakati akiwa kwenye foleni ya kuchyukua matokeo.
  - Samueli anajiaminisha kuwa yeye  ni mjanja na angemshangaza mwalimu mkuu.
  - Anagundua kuwa amefli mtihani huo.  Safu za alama ya D na ilimkodolea macho. Herufi hizo zilimfedhesha na akalwmewa.
  - Nyumbani baba yake aliyengoja matokeo kwa hamu hakuyapata.
  - Samueli anadanganya kwamba ana salio la karo.
  - Baba anarauka na kutembea kilomita sita kwenda kuchukua matoke ya mtihani.
  - Anapogundua ni uwongo anapandwa na ghamiza.
  - Samueli anaamua kujitosa bwawani ili aondokane na athari za kufeli mtihani huu wa kitaaluma.  Hata hivyo amaokolewa na mpita njia.
  - Mama yake anamwambia kuwa ingawa amefeli mtihani wa shule, asikate tama, bado ana mtihani wa maisha ambao anaweza kufaulu.  Anwani hii ina faa sana.

Zozote 10x1

7. Jadili mashaka ya Mashaka  katika hadithi ya “Ndoto ya Mashaka” (alama 20)

- Mhusika Mashaka aliopata mikasa mingi maishani mwake tnagu alipozaliwa.  Kwanza mama yake Ma Mtumwa alifariki alipomkopoa tu, kutokana na kifafa cha uzazi.
- Babake yake naye upweke ulimshinda akafariki na wakazikwa pamoja.
- Mashaka hakuwahi kuwaona hata kwa sura, hivyo hawakumbuki.
- Biti Kidebe ndiye aliyemlea kwa shida na makuzi yalikuwa ya taabu – makuzi ya tikitimaji au tango kuponea umande.

- Biti Kidebe alikuwa haishi kulalamikia miguu yake iliyomuuma. Hivyo, licha yay eye kumlea Mashaka, naye Mashaka akamlea huyu bibi. Alitafuta kila aina ya vijikazi alivyoviweza tangu akiwa motto.
- Biti Kidebe aliwahi kumsomesha kwa shida hadi darasa la nane.
- Alipomaliza shule tu Biti Kidebe akafariki na kumwach mpweke.
- Siku moja akiwa anapiga gumzo na rafiki yake Waridi mlango ulifunguliwa ghafla wakafungishwa ndoa ya mkeka.
- Mashka anapata mke akiwa hana chochote.
- Waliowavamia chumbani mwake ni Mzee Rubeya baba yake Waridi, Sheikh Mwinyumvua, kaka yake Waridi Mansuri na rafiki yake Idi.
- Ndoa hii ilimita Rubeya aibu kwa kuwa binti yake ameolewa na fukara. Mzee Rubeya na familia yake wakaamua kurudi kwao Yemeni.
- Mashaka na Waridi waliishi katika mtaa wa watu wa hali ya chini (fukara) uitwao Tandale.
- Mandhari ya chumba chao kimoja yalikuwa kando ya choo kilichofurika vibaya wakati wa mvua na kueneza kinyesi kila mahali.
- Kulikuwa na uvundo uliotisha kwenye nyumba yao daima.
- Chumba chao kilivuja wakati wa mvua. Wakati huu wanapata tabu sana.
- Mashaka na Waridi walipata watoto saba. Hivyo ilikuwa shida watu tisa kuishi kwenye chumba kimoja.
- Mashaka alikuwa na kazi duni yenye mshahara wa mkia wa mbuzi – alikuwa mlinzi wa usiku katika kampuni za Zuia Wizi Security (ZWS)
- Watoto wake wavulana walilala jikoni kwa jirani Chakupewa.
- Watoto wake wakike walilala chini ya sakafu kwenye mkeka; Mashaka na Waridi walikuwa na vitu vichache sana maana hawakumudu kununua vyombo.
- Nafasi ilikuwa duni kabisa. Ilibidi mkewe apikie nje ya chumba chao isipokuwa, nyakati za mvua ambapo jiko huwekwa juu ya kinu kuzuia maji yanayotiririka.
- Dhiki nyumbani mwa Mashaka ndiyo ilikuwa nguo na harufu yao. Walikuwa na dhiki kubwa sana.
- Siku moja Mashaka aliporudi kutoka kazini alikuta Waridi ametoroka na watoto wote. Toka wakati huo hakuwaona tena. Akabaki mnhyonge na mpweke zaidi.
- Utengano huo ulimfanya ajutie ufukara wake na kuuona kuwa ni udhia mkubwa maishani.
- Mashaka mengi yalijikita akilini mwake kuhusu ukuta na pengo kubwa lililopo katika jamii kati ya walio nacho na wasio nacho.
- Kutokana na shida yake alikuwa na mawazo mazito na maswali yasiyo na majibu – kwa nini jumuiya za kimatiafa zinafumbia macho suala la ufukara?
- Ni ufukara uliomtenginsha yeye na Waridi, yeye na watoto wake na kumwacha katika lindi la maumivu.
- Mashaka alijipa moyo kuwa subira huenda ikamletea heri. Hata hivyo, aliendelea kusubiri akitarajia kuwa mambo yatabadilika. Lakini mambo hayakubzadilika.
- Wakati mwingine aliota ndoto kuwa pengo kati ya maskini na matajiri limepungua, na Waridi mkewe amemrudia Na wote wanaishi kwa furaha. Taabu zake zimepungua mno.

- Kumb hayo yote ni ndoto. Akalazimika kuamka na kupanbana na ulimwengu wake wa mashaka ya umaskini.

Hoja zozote 20 x 1 = 20

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMJULIZI**

8.

a) Fafanua mambo yanayochangia kubadilika kwa fasihi simulizi. (alama 10)
   - Hadhira – fanani awaweza kubadilisha mtindo wake wa utambaji kutegemea hadhira.
   - Wakati – msamiati unafaa wakati wa usimulizi lazima utumike na hivyo kubadilisha fasihi simulizi.
   - Fanani –kila fanani ana njia yake ya uwasilishaji
   - Teknolojia – mambo ya kiasili yanabadilishwa na kuongezewa pia lulingana na mabadiliko ya kiteknolojia.
   - Mazingira – watu wamehama na hakuna pahali pa uwasilishaji maalum. Huwa katika jingo au ukumbi.
   - Video- Fasihi simulizi ina redodiwa katika kanda na uwasilshaji wake ni tofauti na wa fanani (hai)
   - Wakati wa usimulizi – uhalisia unakosekana kwa sababu fasihi simulizi inasimuliwa hata mchana darasani au kumbini.
   - Maandishi – fasihi simulizi imehifadhiwa katika maandishi na hivyo si simulizi ya mdomo tena ni ya kusoma.
   - Mkengeuko – utamaduni hautamaniwi tena na kuishi kuleta mabadiliko katika fasihi simulizi – si muhimu na inasimuliwa kwa nadra sana.
   - Kuingiliana kwa tamaduni – mafanani wanachanganya hadithi za tamaduni tofauti ili kuipa fasihi simulizi uhalisia wote.
   - Uhamaji na uhamiaji – katika harakati hizi mengine yanasahaulika na inabidi kubuni mapya
   - Ukosefu wa utafiti – watu wanajijazia kile wasichokijua kuishi kubadilisha mambo.

   10 x 1 = 10

b) lakabu – Jina la msimbo/ kupanga ambalo mtu hupewa na watu wengine au mtu hujipa mwenyewe
   Hutumiwa badala ya jina lake asilia. (alama 2)

c) Sifa za lakabu
   i. Huonyesha ufanano kati ya jina asilia na mtu
   ii. Huonyesha wasifu wa mtu kwa ufupi
   iii. Husemwa kisirisiri au waziwazi
   iv. Huwa neno moja au fungu la maneno
   v. Huonyesha majigambo ya mhusika
   vi. Ni jina la kijazanda / kiistiari (Simba mwenda pole)
   vii. Hupendelewa hasa na wasanii

   zozote 4 x 1 = 4)

d) Umuhimu wa lakabu

i. Hubainisha sifa ya mtu
ii. Hutumiwa kulinda hadhi ya mtu
iii. Humtambulisha mtu
iv. Hufcsha jina la mtu
v. Huoyesha ubunifu
vi. Hudhihirisha weledi katika lugha husika.
vii. Hudhihaki hali Fulani.
viii. Hufikirisha
ix. Huhamasisha wengine kubuni lakabu zao.
x. Hatambulisha kazi ya msanii.

zozote 4 x 1 = 4